Siku 16 za Uanaharakati 2025

Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia

# Fikiria Upya Mustakabali wa Kifeministi: Kuimarisha Mshikamano, kustawi baada ya Migogoro

## Muhtasari Wa Kampeni

### Kauli mbiu: Pinga. Dai tena. Fikiria upya

## 1. Utangulizi wa Kampeni

Tangu mwaka wa 1991, Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia (UWAKI) imekuwa ni kampeni ya kimataifa ya kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na wasichana, inayotekelezwa kila mwaka kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10. Inawaleta kwa pamoja wanaharakati, jumuiya za kiraia, serikali na taasisi mbalimbali katika kutafuta haki, usalama na usawa. Tangu mwaka wa 2004, Mtandao wa Kuzuia UWAKI umesimamia kampeni hii kwa kuhamasisha wanachama, kuandaa ujumbe wa pamoja, na kupaza sauti ya Wafeministi ili kuongeza uelewa, kushinikiza mabadiliko ya sera, na utetezi wa pamoja.

Mwaka huu wa 2025, tunaimarisha juhudi zetu tukiwa na maono ya mageuzi ya Kifeministi ambayo yanapinga udhalimu hali kadhalika tukifikiria kwa upya ulimwengu ambao wanawake na wasichana wanavyoweza kustawi katikati ya migogoro inayoingiliana: kuhusu anguko la mabadiliko ya hali ya hewa, migogoro ya vita, magonjwa ya mlipuko, ukatili kwa njia ya mtandao, kukosekana kwa usawa wa kiuchumi, na kuongezeka kwa utawala wa kiimla. Pia tunakabiliana na hali mbaya ya kuongezeka kwa vuguvugu la wapinga haki na kupungua kwa ufadhili hali ambayo inatishia mifumo ya huduma na usaidizi ambayo jamii zetu inaitegemea. Hata hivyo, katika hali ngumu, tunashuhudia ustahimilivu— kushirikishana katika mitandao, uendelevu, na kuzidi kusimama katika mshikamano. Mwaka huu, tunaheshimu mapambano na nguvu yetu.

GBV PREVENTION NETWORK

Building Momentum•Fostering Activism

16 DAYS

## 2. Kauli mbiu ya Kampeni ya mwaka 2025: "Fikiria Upya Mustakabali wa Kifeministi, Kuimarisha Mshikamano, kustawi baada ya Migogoro"

Kampeni ya mwaka huu inatoa wito kwa wadau wote kutafakari na kujenga mustakabali imara wa kifeministi uliojikita kwenye haki, uwajibikaji, kujijali, na nguvu ya pamoja. Jinsi migogoro inavyoongezeka, kutoka kwenye mabadiliko ya hali ya hewa hadi ukatili wa mtandaoni, tunasimama kwa pamoja ili kupinga mifumo kandamizi na kujenga mabadiliko ya kudumu.

***Kauli mbiu ya: Pinga. Dai tena. Fikiria upya***

## 3. Malengo ya Kampeni

i. Kurejeshewa mamlaka kupitia uongozi wa Kifeministi kwa kuweka kipaumbele cha kujijali, ujumuishi, na usawa katika juhudi za kuzuia ukatili, kukabiliana na migogoro na kujenga upya jamii.

ii. Kuongeza ufahamu wa kisiasa na wa umma juu ya hitaji la kipaumbele la kujenga mitandao na vuguvugu lenye nguvu la kifeministi ambalo linapaza sauti ya pamoja, ya kupinga, na kuleta mabadiliko ya kina.

iii. Sambaza simulizi za utetezi wa kifeministi kwa kushirikishana hadithi zenye athari chanya na jumbe za utetezi zinazodai mjadala kuhusu haki za wanawake, kusherehekea ushindi wa pamoja, na kuhamasisha umma kuchukua hatua kwa ajili ya haki na usawa.

## 4. Ujumbe wa Msingi wa Kampeni

Ukatili dhidi ya wanawake unatokana na dhuluma ya kimfumo; na inaweza kuvunjwa. Katika hali ya migogoro, vuguvugu la kifeministi huinuka katika mshikamano wa kimkakati na endelevu, unaozingatia uongozi na sauti za wanawake na wasichana katika utofauti wao wote ili kujenga mustakabali wa haki na jumuishi.

## 5. Jinsi Wadau Wanavyoweza Kushiriki

- Kutumia kauli mbiu kutengeneza ujumbe wao, matukio, na kufanya utetezi.
- Kuweka sauti za waliotengwa kwenye utayarishaji wa programu zako.
- Shirikisha hadithi za matumaini, ustahimilivu, na mabadiliko ya kina.
- Shinikiza mabadiliko ya kimuundo katika muktadha unaoendana na eneo lako.
- Imarisha kampeni kwenye mitandao ya kijamii kwa kutumia hashtags na shirikisha kwa njia ya taswira.

# 6. Ufafanuzi kuhusu Kauli Mbiu:

**Kampeni hii inatoa mwito wa kuchukua hatua madhubuti ya kifeministi.** Ni lazima tufanye zaidi ya kushughulikia madhara - lazima tubadilishe mifumo inayosababisha hali hii. Huku tukishuhudia ongezeko la migogoro, upinzani mkali, na kutokuwepo na usawa, vuguvugu dhabiti la utetezi wa haki za wanawake lililojikita kwenye jamii ili kujenga mustakabali wa haki na ukombozi.

Fikiria upya mifumo ya Kifeministi. Tunajenga upya miundo kwa ajili ya kutoa haki. Kwa maana kwamba kubadilisha mifumo ya utawala, haki, na uchumi kwa kuzingatia huduma, uwajibikaji, na ushirikishwaji. Mifumo ya kifeministi inathamini kazi za huduma zisizo na malipo, kuwekeza kwenye kutoa huduma kwa kijamii, na kuwarejeshea mamlaka wale ambao historia imewatenga

Himiza ushirikishwaji, huduma, na mgawanyo mpya wa rasilimali. Tunadai mifumo ambayo wanawake na jamii wana ushawishi katika kufanya maamuzi. Tunatoa kipaumbele katika mshikamano na kutoa huduma kuliko kupata faida, na tunatoa msukumo juu ya haki ya kiuchumi kupitia mgawanyo mpya wa rasilimali na mamlaka.

Inua mshikamano, ustawi kupitia mabadiliko ya kina. Kampeni hii inahusu kuinuka kwa pamoja, kuvuka mipaka, vizazi, na utambulisho; kalaani upinzani na kujenga mustakabali wa baadae ambao wanawake wote, wasichana, na watu wa jinsia tofauti wanaweza kustawi. Tunatenda kwa matumaini dhabiti, tukijua kwamba mabadiliko si tu ni ya lazima, bali yanawezekana.

# 7. Wito wa Kuchukua Hatua

- **Wito wa Kuchukua Hatua kwa Mtu Binafsi:** Tumia sauti yako—mtandaoni na nje ya mtandao—kukuza vuguvugu la utetezi wa haki za kifeministi, ili kupinga kutokuwepo na haki, na kusimama pamoja na wahanga na makundi yaliyotengwa. Kuwa na mazoezi ya kutoa huduma na ushirikeli kama hatua madhubuti ya mshikamano. Shiriki katika kampeni za ndani, saidia juhudi zinazoongozwa na jamii, na kuunganisha hatua utakazochukua na mapambano ya kimataifa ya utetezi wa haki na usawa.
- **Wito wa Kuchukua Hatua kwa Mashirika na Wadau wa Maendeleo:** Wakati wa Siku 16 za Uanaharakati, chukua hatua za kijasiri ili kutetea haki ya kijinsia kwa kutoa ufadhili kwa vikundi vinavyoongozwa na wanawake kwa njia inayonyumbulika, hamisha mamlaka kwa viongozi waliotengwa, imarisha muungano wa vuguvugu mbalimbali, na kutoa kipaumbele kwenye huduma na usalama ili kudumisha hatua ya muda mrefu ya utetezi wa haki za kifeministi.
- **Wito wa Kuchukua Hatua kwa Jamii:** Fanya kazi kwa kushirikiana na wahanga ili kujenga kwa pamoja sehemu salama, ya uponyaji iliyoandaliwa kutoka na mahitaji yao. Tumia sanaa, mazungumzo, na ushirikishwaji wa jamii ili kupinga kanuni potofu za kijinsia. Weka kipaumbele kwenye kutoa huduma kwa kujenga mifumo ya usaidizi ya kijamii ambayo inaimarisha usalama na uponyaji zaidi ya adhabu na kutumia nguvu.

- **Wito wa Kuchukua Hatua kwa Serikali:** Wakati wa Siku 16 za Uanaharakati, wito kwa serikali ni lazima zichukue hatua za kijasiri na za kimfumo kwa kuchukua hatua madhubuti zinazoongozwa na jamii, zinazozingatia maslahi ya wanawake; kuongeza ufadhili katika taifa ili kuzuia ukatili na kutoa huduma kwa wahanga; na kulinda nafasi ya kiraia huku ikishirikiana na vuguvugu la kifeministi ili kuunda sera zilizo jumuishi, na zenye uwajibikaji.

**Jiunge na Kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati ya mwaka 2025: Hashtags Rasmi:** #FeministFutures | #16DaysOfActivism | #EndOnlineViolence